

Janet T. Mills
Governor

Jeanne M. Lambrew, Ph.D.
Commissioner



Maine Department of Health and Human Services
Child and Family Services
11 State House Station
2 Anthony Avenue
Augusta, Maine 04333-0011
Tel.: (207) 624-7900; Toll Free: (877) 680-5866
TTY: Dial 711 (Maine Relay); Fax: (207) 287-5282

KUMBUKUMBU

- KWA:** Familia na watoaji wa programu ya ruzuku ya watoto
- KUTOKA:** Ofisi ya huduma za Watoto na Familia
- TAREHE:** Agosti 25, 2021
- KUHUSU:** Ulipaji wa Mpango wa Ruzuku ya Watoto kulingana na Sasisho la Mahudhurio

Programu ya Ruzuku ya kusaidia watoto (CCSP) ya Huduma ya Watoto na Familia (OCFS) ilianza kulipa kulingana na uandikishaji dhidi ya mahudhurio mnamo 03/27/21 hadi 09/25/21. OCFS inafurahi kutangaza kwamba kupitia Sheria ya Mpango wa Uokoaji wa Amerika (ARPA), Fedha za hiari za CCDF Maine ilipokea, tutakuwa tukiendeleza faida hii kupitia 9/30/23 au hadi wakati fedha hazipatikani tena.

Kama ukumbusho:

- Watoaji huduma wanaweza kulipisha hadi saa za juu kwenye barua ya tuzo ya mtoto, iwe mtoto anakuja au haji.
- Wakati Mtoto hayupo kwenye mpango zaidi ya wiki mbili (2) mfululizo kwa sababu hiyo hiyo inayofaa, Mtoa Huduma ya Mtoto lazima apate idhini ya maandishi kutoka Idara ili kuendelea Malipo ya Ruzuku ya Huduma ya Mtoto.
- Bado wazazi wanahitaji kuripoti kutokuwepo, kwa mtoa huduma wao. Kutokuwepo kwa njia isiyokubalika kunamaanisha kutokuhudhuria kwa Mtoto katika Huduma ya Mtoto kwa zaidi ya siku mbili (2) za kalenda kwa mwezi bila sababu au idhini ya awali kutoka kwa Idara.

Watoa huduma lazima bado wakamilishe fomu za malipo. Masaa ya kawaida yatakuwa masaa halisi mtoto anahudhuria na masaa ya msamaha yatakuwa masaa yaliyoongezwa ili kumfikisha mtoto kwenye idhini kubwa inayoruhusiwa kama inavyoidhinishwa kwenye barua ya tuzo.

- Mfano: Jane Doe ni mtoto wa umri wa kwenda shule na amepewa ruzuku hadi saa kamili (masaa 30). Jane kawaida huhudhuria utunzaji wa watoto wakati wote wa sama au majira ya joto, na mara kwa mara wakati wa wa shule, Jumatatu saa moja – saa mbili asubuhi, Jumanne saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni, Jumatano saa moja - mbili asubuhi, Alhamisi saa mbili asubuhi hadi saa kumi na moja jioni, Ijumaa saa moja – saa mbili asubuhi kwa jumla ya masaa 21 kwa wiki. Fomu ya kulipia wakati wa mwaka wa shule ingeonyesha masaa 21 ya kawaida na masaa 9 za udhuru kuongeza hadi masaa 30 ya wakati wote.

Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali tuma barua pepe CCSP.DHHS@maine.gov au piga simu 624-7999.